**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam**
**1 Novemba 2008**

**Waliohudhuria**
Ally Athuman Jumbe
Ally Saidi Mwishehe
Bashiri Rashidi
Dominata Rwechungura
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rwechungura
George Kabogo
Husein Hamza Hamisi
Idrisa Kessi Zongo
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Hassan Chibaya
Mohammed Hamidu
Paulo Atibu Hatibu
Ramadhani Rajabu Nyengo
Shamte J Kigoma
Sosthenes C Amlima
Sudi Saidi Ramadhan

**Wageni**

| | |
|---|---|
| Ragna Schmidt-Haupt | Cycle Generation |
| Amiram Roth-Deblon | Cycle Generation |
| Johannes Hahn | TASEA |

**Msafara wa Baiskeli**
Msafara wa Baiskeli ulienda vizuri sana. Watu 150 walishiriki. Azzan Zungu, Mbunge alitoa hotuba kama mgeni rasmi na Diwani Lupilya aliendesha baisikeli kwenye msafara. Wanawake wawili kutoka Kali Mata walishirika. Watu wanne waliendesha roller-blades pia.

Mwendesha roller-blades alishinda guta la abiria lililochangiwa na kampuni ya guta. Husein Hamza alishinda California bike moja, nyingine mlevamu alishinda na nyingine ilishindwa na mpanda baisikeli mwanamume. Baisikeli ya mlemavu ilishindwa na mlemavu kutoka Kigamboni.

Channel 10 na DTV walionyesha Diwani Lupilya akiongea kuhusu masuala ya baisikeli Dar es Salaam. Sunday Citizen waliweka picha ya msafara ukurasa wa kwanza na Mussa na Sosthenes walikuwa ndani ya picha. Majira waliandika makala lakini hakuna mwanachama aliyenunua – Sosthenes atajaribu kupata wiki hii.

**Wageni**
Wageni walijitambulisha – wote watatu ni wagerumani.

Wapanda baisikeli wawili kutoka “Cycle Generation” wameendesha baisikeli hapa kutoka Ethiopia kwa miezi sita na wataendelea mpaka Afrika Kusini. Lengo ni kupiga kampeni kuhusu mabadaliko ya majira kwenye masuala matatu – mishati, misitu na usafiri/baisikeli. Wametembelea mashirika mengi kwenye nchi ambazo wameshatembelea - Ethiopia, Kenya, Rwanda, Uganda, Congo na Tanzania. UWABA ni shirika la kwanza linalohusika na baiskeli wamekutana nalo. Tuliwapa namba ya simu kwa ofisi ya Naibu Rais waliotupokea siku la uamsho wa mabadaliko ya majira mwaka jana. Walifanya intavu na video kwa kiingereza na Sosthenes na Filbert. Walisema watatangaza UWABA kwenye website na wakati wanaongea na waandishi wa habari.

Johannes anajitolea kwa TASEA – anafanya kazi kuhusu masharti ya safi ya mazingira. Atakaa mwaka mmoja na yupo wiki mbili mpaka sasa. Ana mpango kuendesha baiskeli Dar es Salaam na atajiunga na UWABA.

**Morogoro**
Filbert, Bashiri na Edgar walienda Morogoro kwa ajili ya kufundisha usalama wa baiskeli chini ya mradi wa Wizara ya Miundombinu. Lakini walipofika waliona hawajatangaza vizuri na hawajatoa taarifa kwa shule, hawajaweka sehemu kwenye uwanja, hawakupewa nafasi kwenye ratiba na wanafunzi wapanda baiskeli walikuwa kumi na hakuwa tayari kwa mafunzo walikuja kwenye tukio kuangalia tu. Hata MC aliwaambia wapanda baiskeli kutoka ili Waziri Mkuu awe na nafasi kupita.

Allan aliomba samahani na alisema atahakikisha matayarisho yatakuwa mazuri mara nyingine. Alitupa reflecta alizonunua kama zawadi – zingine tulisambaza kwa wanachama na zingine Juma anabaki nazo kama zawadi za baadaye.

**Video ya Usalama Barabarani**
Amar alimaliza kufanya editing ya video ya usalama barabarani na alitumia kwa email. Elaine alidownload akaangalia lakini hakuweza kusikia kwa sababu hana spika kwenye kompyuta kazini. Tulijaribu kuangalia pamoja kwenye internet café lakini meneja hakuwepo na hutukuruhusu. Tutaiangalia siku nyingine.

**Mradi wa Wamba**
Elaine atawasiliana na shule wiki hii ili kuandaa tarehe ya mafunzo.

**Kongamano**
Elaine ataandika proposal ili tutumie kwenye idara mbali mbali za serekali.

**Mambo ya hela**
Ally Saidi Mwishehe alileta Tsh 20,000 ya kodi ya guta ya wiki tatu bila siku la msafara ambapo guta lilitumikwa kwenye msafara.

Tuliandika mambo ya hela ya msafara na Elaine ataandika kwenye repoti. Elaine sasa ana Tsh 144,300 ya hela ya UWABA, Juma ana Tsh 67,500 (ndani kuna Tsh 1,200 alikuwa nayo kabla ya msafara na Tsh 20,000 aliyopokea leo ya kodi ya guta) na Mejah alitumia balance yote yake ya UWABA.